KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

KISWAHILI GREDI LA TISA

MTIHANI WA KATIKATI YA MUHULA WA PILI 2026

JINA……...NAMBARI YA USAJILI……

SEHEMU YA KWANZA: UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 6:

Magonjwa yasiyoambukizwa ni magonjwa ambayo hayaenezwi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Hii ni kwa sababu hayana vimelea kama vile virusi vinavyoweza kusambazwa. Takwimu za shirika la Afya duniani zinaonyesha kuwa magonjwa haya yanaongezeka kwa kasi sana na kuathiri watu wengi ulimwenguni.

Magonjwa haya ni kama vile: saratani, ugonjwa wa kisukari, shinikizo la damu na kadhalika. Magonjwa yenyewe husababishwa na mabadiliko ya mitindo ya maisha kama vile kutofanya mazoezi hasa kwa watu wanaoketi kwa muda mrefu bila kushiriki mazoezi yoyote, ulaji wa vyakula visivyofaa ambapo watu hula lishe isiyoendana na mahitaji ya mwili. Pia kula mafuta na chumvi zaidi ya mahitaji ya mwili kutokula mboga na matunda kiasi cha kutosha ni baadhi ya visababishi vya magonjwa hayo. Aidha, unywaji wa pombe na uvutaji sigara vilevile husababisha magonjwa kama haya. Nchi zinazoendelea zinajitahidi katika malengo endelevu ya dunia ikiwemo lengo la tatu linalosisitiza kuhusu afya bora. Ni muhimu kujua mbinu za kujikinga kutokana na magonjwa hayo.

1. Kulingana na kifungu, ni kweli kuwa:

A. Magonjwa yasioambukizwa yanaweza kuenezwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine.
B. Magonjwa yasiyoambukizwa huwa na vimelea ambao wanaweza kusambazwa.
C. Magonjwa yasiyoambukizwa hayawezi kupitishwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine.
D. Magonjwa yasiyoambukizwa husababishwa na virusi vinavyoweza kusambazwa.

2. Kwa mujibu wa kifungu, magonjwa haya hayawezi kuambukizwa isipokuwa:

A. Ugonjwa wa saratani.
B. Ugonjwa wa waba.